TAARIFA YA MKUU WA CHUO, PROF. SHADRACK S. MWAKALILA, KWA MHE. KIPANGA JUMA OMARY (Mb) NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

WAKATI WA ZIARA KATIKA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE, KIVUKONI, TAREHE 8 JANUARI, 2021

Mheshimiwa KIPANGA JUMA OMARY (Mb)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Mheshimiwa Steven Masato Wasira,

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo;

Ndugu Viongozi na Wafanyakazi wa Chuo;

HERI YA MWAKA MPYA WA 2021!!

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Awali ya yote Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi MUNGU kwa kutuwezesha kuwepo hapa katika siku ya leo. Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Magufuli kuwa Naibu Waziri wa elimu sayansi na teknolojia.

Pia tunakushukuru kufanya ziara ya kikazi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Ni dhahiri kuwa una majukumu mengi yaliyo mbele yako, lakini umeamua kutenga muda wako kuja kutembelea Chuo hiki. Ujio wako unadhihirisha jinsi unavyokithamini Chuo hiki cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Chimbuko la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni Chuo cha Kivukoni ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 29 Julai 1961. Uamuzi wa kuanzisha Chuo hiki ulikuwa ni uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Chama cha TANU wa Tabora 1958. Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuandaa viongozi. Aidha, Katika kipindi cha mwaka 1972 hadi 1992, Chuo hiki kilikuwa chini ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na kilikuwa na vyuo vya Kanda Nane (8) katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Nchi yetu ilipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, Mwaka 1992, Chuo kilianza kumilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Chuo hiki kilipewa jina la Mwalimu Nyerere kwa lengo la kuendelea kumuenzi Baba wa Taifa ambaye alifanya kazi kubwa ya ukombozi wa Taifa letu, ukombozi wa Afrika na kuwatetea wanyonge popote duniani. Aidha, Hayati Mwalimu Nyerere, ndiye aliyekuwa muanzilishi wa Chuo hiki, wakati huo kikiitwa Chuo cha Kivukoni. Chuo kina kampasi mbili- Kampasi ya Kivukoni (Dar es Salaam) na Kampasi ya Karume (Zanzibar). Aidha, Chuo kilifungua Tawi Pemba ambalo lilianza kutoa mafunzo tarehe 16 Marchi2020 kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wahitaji ikiwa ni pamoja na kufungua matawi katika kanda za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Dira ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni kuwa kitovu cha utoaji wa maarifa bora kwa kutoa elimu na mafunzo kuhusu ubunifu na uvumbuzi na kuendeleza amani na umoja wa kitaifa.

Hivyo Majukumu makuu ya Chuo ni pamoja na:

(a) Kutoa mafunzo katika fani mbalimbali za Sayansi Jamii kwa kiwango cha Astashahada, Stashahada na Shahada;

(b) Kutoa mafunzo ya Uongozi, Maadili, Uzalendo na Utawala bora;

(c) Kuendesha mafunzo ya Elimu ya Kujiendeleza;

(d) Kufanya utafiti zenye kutatua changamoto mbalimbali za kijamii;

(e) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta za umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Chuo hiki kina historia ya kuendesha mafunzo ya uongozi katika ngazi zote za uongozi katika Taifa letu na kwa viongozi wa aina mbalimbali ndani ya Nchi na Nje ya Nchi. Hivyo kwa sasa mbali na kutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali za kitaaluma, Chuo kinatoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Maadili yanayokidhi mahitaji ya makundi mbali mbali ya viongozi kuanzia ngazi ya kijiji/kata, Wilaya, mkoa hadi Taifa ili kuwajengea weledi, Utaifa, Uzalendo, Uadilifu na Uongozi bora kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Chuo kimepata mafanikio mengi katika kipindi cha kwanza cha serikali ya awamu ya tano (2015-2020) chini ya uongozi wa Mhe. Dkt John Pombe Magufuli, kama ifuatavyo:

1) Chuo kiomeongeza udahili wa wanafunzi ambapo katika Kampasi ya Kivukoni udahili umeongezeka kutoka wanafunzi 1570 mwaka 2015 hadi 9,754 mwaka 2020. Aidha katika Kampasi ya Karume-Zanzibar pia udahili umeongezeka kutoka wanafunzi 22 mwaka 2015 hadi 1,659 mwaka 2020. Hivyo kwa ujumla idadi imeongezeka kutoka wanafunzi 1592 wa mwaka 2015 hadi wanafunzi 11,413 mwaka 2020.

2) Chuo kiomeongeza idadi ya wahitimu ambapo Katika Kampasi ya Kivukoni idadi ya wahitimu imeongezeka kutoka wahitimu 569 katika mwaka wa masomo 2014/2015 hadi kufikia wahitimu 3,925 katika mwaka wa masomo 2020/2021. Aidha, Katika Kampasi ya Karume mwaka 2020 wahitimu walikuwa 771. Hivyo jumla ya wahitimu wote wa 2020 walikuwa **4,696.**

3) Chuo kiomeongeza Idadi ya watumishi kutoka watumishi 168 mwaka 2015, hadi watumishi 285 ambapo kati yao Kampasi ya Kivukoni-Dare Salaam wapo 231 na Kampasi ya Karume, Zanzibar wapo 54.

4) Chuo kiomeongeza Idadi ya waalimu/Wahadhiri wenye shahada ya uzamivu (PhD) kutoka wahadhari 2 wenye PhD

mwaka 2015 hadi Wahadhiri 35 mwaka wa 2020. Mwaka 2021 watakua zaidi 40 baada ya kuhitimu PhD.

5) Chuo kimeongeza Idadi ya programme za mafunzo ya kitaaluma kutoka programme 3 za shahada zilizokuepo mwaka 2015 hadi kufikia jumla ya programme 10 za shahada na Programme moja ya Shahadi ya Umahili (Masters Degree) mwaka 2020. Kwasasa Chuo kina programme 10 ngazi ya Shahada, programme 11 ngazi ya Stashahada (Diploma) na programme 11 ngazi ya Astashahada (Certificate) kwa maelezo zaidi Rejea tuvuti ya Chuo: www.mnma.ac.tz.

6) Chuo kimeboresha Mitaala yote ikiwa ni pamoja na kuingiza somo la uongozi, Maadili, na uzalendo katika Mitaala yote ili kila mwanafunzi awe na ufahamu wa kutosha kuhusu Uongozi, Maadili, na Uzalendo. Aidha, Chuo kimejipanga kuwa kitovu bora cha mafunzo ya uongozi na Maadili yaani (Centre of Excellency).

7) Chuo kimefanikiwa Kuongeza idadi ya vitabu zaidi ya 20,000 katika maktaba zote za chuo katika kampasi zote za Chuo.

8) Chuo kimekamilisha ujenzi wa ukumbi wa Mihadhara (Lecture Theatre) wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa pamoja, na ofisi 10 za wafanyakazi. Ujenzi ulianza mwaka 2017 na kukamilika mwaka 2019.

9) Chuo kimekamilisha ujenzi wa Hostel ya wanafunzi ambao ulikuwa umesimama tangu mwaka 2014 kwa sababu ya kukosa fedha za maendeleo. Hostel hii mpya ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 720.

10) Chuo kimeboresha Mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi ikiwa ni pamoja na uwekaji wa viti visivyo hamishika (fixed chairs) kwenye kumbi zote, ufungaji wa vifaa vya kisasa (projectors) katika kumbi za mihadhara, ununuzi wa computer kwa ajili ya Maabara za Computer.

11) Chuo kimenunua magali manne (6) mapya kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Chuo.

12) Chuo kimefanikiwa kupeleka wahadhiri zaidi ya 40 katika mafunzo ya shahada ya uzamivu katika fani mbalimbali za kitaaluma. Aidha, watumishi katika idara mbalimbali za

kitaaluma na uendeshaji wamejengewa uwezo kupitia mafunzo ya muda mfupi.

13) Chuo kimefanikiwa kutatua changamoto ya mmomonyoko wa eneo la ufukwe wa bahari, kwa msaada wa ofisi ya Makamu wa Rais ambayo ilijenga ukuta na kuweka eneo katika mazingira ya kuweza kutumika na wanafunzi pamoja na jamii ya chuo.

14) Chuo kimefanikiwa kutoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi, maadili, utawala bora na uzalendo kwa watendaji mbalimbali wa serikali. Aidha wahitimu wa chuo walipewa mafunzo maalumu ya uongozi, maadili, uzalendo na utawala bora, zaidi ya wanafunzi 3,000 wamepata mafunzo haya.

15) Chuo kimefanikiwa kujenga na kuimarisha mahusiano mazuri ya kitaaluma na taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

16) Chuo kupitia idara ya TEHAMA kimefanikiwa kutoa bunifu Ishirini na mbili (22) kwa mwaka wa masomo 2019/2020. Aidha chuo kilifanikiwa kupeleka wanafunzi

watano (5) wenye bunifu mbalimbali katika mashindano ya kitaifa ya Sayansi Tekonolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika Marchi 2020. Mwanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere MUHAMED RAMADHAN aliyebuni na kutengeneza mfumo wa kutambua na kudhibiti upotevu wa gesi kutoka katika mtungi wake alikuwa mshindi wa pili katika kundi la vyuo vya elimu ya ufundi vya kati.

17) Chuo kimefanikiwa kutenga bajeti na kuanza mchakato wa ujenzi wa Hostel katika kampasi ya Karume-Zanzibar itakayo kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1536.

18) Chuo kimefanikiwa kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Maktaba katika kampasi ya Kivukoni-Dar es Salaam itakayo kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2500.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Pamoja na mafinikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 5 ya awamu ya tano, chuo kimejipanga kutekeleza ipasavyo maelekezo ya Serikali kwa kuzingatia Ilani ya CCM ikisomwa pamoja na Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Pombe Magufuli wakati wa kufungua rasmi bunge la 12 la Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania Dodoma, tarehe 13 Novemba, 2020. Aidha Chuo kimejipanga kusimamia ipasavyo ukusanyaji wa maduhuli na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kusaidia kudumisha na kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa NAIBU WAZIRI,

Kwa mara nyingine, tunakushukuru kwa kutembelea Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. MUNGU AKUBARIKI!!!.

Prof. Shadrack S. Mwakalila.

MKUU WA CHUO